



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO
YA AMALI**

MHE. LELA MUHAMED MUSSA (MBM)

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA
FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

Mei, 2025



Mhe. Lela Muhammed Mussa
Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
Zanzibar



Mhe. Ali Abdulgulam Hussein
Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
Zanzibar



Mr. Khamis Abdulla Said
Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
Zanzibar



Mr. Khalid Masoud Wazir
Naibu Katibu Mkuu Utawala
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
Zanzibar



Dkt. Mwanakhamis Adam Ameir
Naibu Katibu Mkuu Taaluma
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya
Amali

YALIYOMO

UTANGULIZI.....	1
MIRADI YA SEKTA YA ELIMU	5
UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025	5
MUUNDO WA PROGRAMU	5
UTEKELEZAJI WA MPANGO WA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025	5
PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI	7
PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.....	10
PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU	13
Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu.....	14
Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti.....	16
Huduma ya Sayansi na Teknolojia.....	19
Huduma ya Teknolojia - IIT Madras.....	21
Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu	22
Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu.....	24
PROGRAMU YANNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI	27
Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima.	27
Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali	29
PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU.....	31
Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia	32
Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu	34
Huduma ya Ukaguzi wa Elimu.....	36
Huduma za Maktaba.....	38
Huduma ya Baraza la Elimu	40
ProgramundogoyaTeknolojiayaHabarinaMawasilianokatikaElimu .	41
Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha.....	44
Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli	45
PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI.....	47
Programu ndogo ya Uongozi Kiujumla.....	48
Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti.....	49

<u>Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Mwaka 2025/26</u>	ii
Programu ndogo ya Uratibu shughuli za elimu Pemba	52
MAPATO	52
MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2025/2026 KATIKA MFUMO WA PROGRAM	53
Vipaumbele vya Wizara	53
MAELEZO YA PROGRAMU ZA ELIMU.....	56
PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI	56
PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.....	57
PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU	58
Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu.....	59
Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti.....	60
Huduma ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia	61
Huduma ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.....	62
Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu.....	62
PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI	63
Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima	63
Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali	64
PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU.....	65
Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia.....	65
Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu	66
Huduma ya Ukaguzi wa Elimu	66
Huduma za Maktaba	67
Huduma ya Baraza la Elimu.....	68
Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha	69
Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).....	69
Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli ...	70
PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI.....	71
Programu ndogo ya Uongozi kiujumla	71

<u>Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Mwaka 2025/26</u>	iii
Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango,	
Sera naUtafiti.....	72
Programu ndogo ya kuratibu shughuli za Elimu Pemba	73
MAKADIRIO YA MAPATO	73
JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI.....	74
SHUKURANI	74
KIAMBATISHO	76

**HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA
FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

UTANGULIZI

- 1. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liingie katika Kamati ili niweze kutoa maelezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2025/2026.
- 2. Mheshimiwa Spika**, Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma na Mwenye Kurehemu kwa kuturuzuku neema ya uhai na afya njema tukaweza kukutana tena katika kikao hiki cha kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Namuomba anijaalie ufasaha katika kuiwasilisha hotuba hii na pia awawezeshe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kuichambua kwa kina, kuichangia na hatimaye kuipitisha kwa kauli moja kwa manufaa ya taifa letu.
- 3. Mheshimiwa Spika**, Nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati viongozi wetu wakuu; Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa, Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kudumisha umoja, amani ya nchi yetu na kuwaleta wananchi Maendeleo. Sote ni mashahidi wa mageuzi makubwa ndani ya kipindi kifupi, ambayo yameimarisha mifumo na kukuza ubora wa elimu inayotolewa kwa kiasi kikubwa. Aidha, malengo

na maazimio ya kitaifa na kimataifa yametekelawa kwa mafanikio makubwa, huku tukivuka shabaha za malengo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Aidha, napenda kutoa pongezi maalum kwa Mama Maryam Mwinyi, Mke wa Rais wa Zanzibar, kwa michango mbalimbali anayotupatia kupitia taasisi ya Maisha Bora Foundation katika kuimarisha ubora wa elimu Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika**, Neema alizotuahidi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zimekamilika. Bila shaka wananchi wategemee neema zaidi katika kipindi chake cha pili cha miaka mitano cha Serikali ya awamu ya nane. Niwaombe wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla washiriki uchaguzi kikamilifu kwa amani na niwatakie viongozi wetu ushindi mnono, Mwenyezi Mungu awajaalie afya njema, hekima, busara na maarifa zaidi ili waendelee kutuongoza kwa ufanisi mkubwa na kutuletea maendeleo zaidi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Napenda kutoa pongezi na shukurani za dhati kwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud Othman, na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa utendaji wao mzuri katika kuleta maendeleo ya Zanzibar.
5. **Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa hii adhimu kukupongeza wewe binafsi, pamoja na Naibu Spika na Mwenyekiti wa Baraza la wawakilishi kwa umahiri, hekima na weledi mkubwa mnaouonesha katika kuliongoza Baraza hili tukufu. Uongozi wenu umeendelea kuwa dira na mwanga katika kuhakikisha mijadala na hoja zinazowasilishwa humu zinazingatia maslahi mapana ya wananchi wetu na

mustakabali wa Taifa kwa ujumla. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwaongeza hekima, busara na ujasiri wa kuendelea kusimamia haki, uwazi na ustawi wa watu wa Zanzibar. Aidha, shukrani za kipekee ziende kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wote wa Baraza kwa utekelezaji wao mzuri wa majukumu ya kila siku na kuhakikisha kuwa shughuli za Baraza zinaendeshwa kwa ufanisi mkubwa na kwa viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

6. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti wao shupavu, Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani. Ni wazi kuwa kamati hii imekuwa si tu mfuatiliaji, bali mshiriki hai wa mabadiliko tunayoendelea kuyaona kwenye sekta ya elimu. Sambamba na hilo, nawashukuru Wenyeviti na wajumbe wa Kamati zote za Baraza hili kwa kazi kubwa na mchango wao wa kipekee katika kuhakikisha kuwa mipango ya Serikali inazingatia uhalisia wa mahitaji ya wananchi.
7. **Mheshimiwa Spika**, kwa unyenyekevu na moyo wa shukrani, napenda kutoa pongezi za dhati kwa watendaji wote wa Taasisi ya Afisi ya Rais Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini (PDB), chini ya uongozi thabiti wa Mtendaji Mkuu wao, Profesa Mohammed Hafidh Khalfan. Ushirikiano wao wa karibu umeendelea kuwa nguzo muhimu katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati hususan katika sekta ya elimu.
8. **Mheshimiwa Spika**, Nichukuwe fursa hii pia kumshukuru na kumpongeza Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya

Amali Mheshimiwa Ali Abdulghulam Hussein kwa kunipa mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii. Pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wakiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Utawala, Naibu Katibu Mkuu Taaluma, Afisa Mdhamsini wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi mbalimbali za Elimu, Maafisa wa ngazi mbalimbali wa Wizara, bila kusahau walimu na Kamati zetu za skuli kwa mashirikiano yao makubwa katika kuleta maendeleo ya elimu nchini. Aidha, shukurani ziwafikie wazazi, wanafunzi na wadau wote wa elimu wa ndani na nje ya nchi kwa ushiriki na michango yao katika kusaidia harakati za utoaji na upatikanaji wa huduma ya elimu bora. Mwenyezi Mungu awazidishie moyo wa imani na uzalendo kwa nchi yetu.

9. **Mheshimiwa Spika, Mwisho nawashukuru sana watendaji** wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Tume ya Mipango, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mkaguzi Mkuu wa Ndani, ZAECA, Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na Taasisi nyengine kwa ushirikiano wao ambao umechangia katika kuimarisha huduma za elimu katika mwaka 2024/2025. Ni matumaini yetu kuwa ushirikiano huo utaimarika zaidi katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za elimu bora katika Taifa letu.
10. **Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuelezea matarajio ya bajeti ya mwaka 2025/2026, nitawasilisha utekelezaji wa mpango wa elimu kwa Mwaka wa fedha wa 2024/2025.

MIRADI YA SEKTA YA ELIMU

11. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ilitekeleza kazi zake kupitia miradi mikuu mitatu kama ifuatayo:

- i. Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu katika elimu
- ii. Mradi wa Uimarishaji wa Ubora wa Elimu
- iii. Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu

UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025

12. Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuwasilisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 kupitia programu sita za elimu.

MUUNDO WA PROGRAMU

13. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina jumla ya programu kuu sita kama zifuatazo: -

Programu ya Kwanza: Elimu ya Maandalizi na Msingi

Programu ya Pili: Elimu ya Sekondari

Programu ya Tatu: Elimu ya Juu

Programu ya Nne: Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali

Programu ya Tano: Ubora wa Elimu

Programu ya Sita: Uongozi na Utawala

UTEKELEZAJI WA MPANGO WA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025

14. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu kwa mwaka wa fedha 2024/2025 umezingatia malengo ya maendeleo ya elimu ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050, Mpango wa Maendeleo ya kitaifa 2021-2026,

Vipaumbele vya sekta, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Maagizo ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, pamoja na Mipango mengine ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

15. **Mheshimiwa Spika**, Programu hizo zote zilitengeza kwa mashirikiano makubwa kati ya Serikali, Washirika wa Maendeleo wa ndani na nje ya Zanzibar pamoja na Jamii kwa ujumla. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu hizi zilitengewa jumla ya **Tsh. 830,955,702,000** kati ya fedha hizo **Tsh. 618,400,398,000** ni kutoka SMZ na **Tsh. 212,555,304,000** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa upande wa fedha za SMZ, **Tsh. 308,794,998,000** zilitengwa kwa ajili ya kazi za Maendeleo na **Tsh. 309,605,400,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida yanayojumuisha **Tsh. 213,900,000,000** za mishahara, **Tsh. 45,491,700,000** za matumizi mengineyo na **Tsh. 50,213,700,000** kwa ajili ya ruzuku kwa Taasisi za Wizara zinazopokea ruzuku. Aidha, kwa upande wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo **Tsh. 209,269,914,000** ni kwa ajili ya kazi za Maendeleo na **Tsh. 3,285,290,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.
16. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 409,729,646,068** sawa na asilimia **49** ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 175,967,128,973** sawa na asilimia **82** zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na **Tsh. 26,800,968,878** sawa na asilimia **55** zimetumika kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **Tsh. 167,272,787,830** sawa na asilimia **32** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 115,920,114,523** sawa

na asilimia 38 ni kutoka SMZ na **Tsh. 51,352,673,307** sawa na asilimia **25** ni kutoka kwa wahisani ambapo shughuli nyingi za Miradi ya Wahisani zinategemea kukamilika kwa taratibu za Manunuzi zinazoendana na miongozo yao.

- 17. Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji halisi kwa kila Programu ni kama ifuatavyo: -

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

- 18. Mheshimiwa Spika**, Programu hii inahusisha uimarishaji na utoaji wa elimu ya maandalizi na msingi kwa wanafunzi wenyewe umri wa kuanzia miaka minne hadi kumi na mbili.
- 19. Mheshimiwa Spika**, Programu hii ilitengewa jumla ya **Tsh. 236,293,613,698** Kati ya fedha hizo **Tsh. 117,599,363,698** ni kwa ajili ya kazi za kawaida zikiwemo **Tsh. 108,179,568,000** za Mishahara, **Tsh. 9,419,795,698** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Tsh. 118,694,250,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 153,348,594,171** sawa na asilimia 65 ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 86,391,485,604** sawa na asilimia 80 zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na **Tsh. 6,974,470,303** sawa na asilimia **74** zimetumika kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **Tsh. 59,982,638,264** sawa na asilimia 51 zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 57,401,923,395** sawa na asilimia **62** ni kutoka SMZ na **Tsh. 2,580,714,869** sawa na asilimia **10** ni kutoka kwa wahisani. Fedha hizo zilitumika kutekeleza shughuli zifuatazo: -

- i) Jumla ya Skuli 97 za Maandalizi na Msingi Unguja na Pemba zinaendelea kufanyiwa Ukarabati, ambapo

skuli 17 za Mkoa wa Mjini Magharibi zimekamilika na Skuli 80 katika mikoa mingine ukarabati unaendelea.

- ii) Ujenzi wa skuli 21 za Maandalizi unaendelea katika maeneo ya Fuoni Kipungani, Dole, Sharifumsa, Kitogani, Kizimkazi Dimbani, Koani, Jumbi, Kitope, Donge, Kibuyuni, Kinyasini, Mbuzini kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba katika maeneo ya Mtimbu, Kangani, Mkoani, Mitiulaya, Kivugo, Maziwang'ombe na Karume.
- iii) Ujenzi wa skuli 15 za Msingi zikiwemo skuli 14 za chini unaendelea katika maeneo ya Mwera Mtifaani, Potoa Msingi, Vuga Mkadini, Ziwani, Kipitacho, Michenzani, Ndongini Wambaa, Kiungoni, Kojani, Kizimbani, Kiuyu, Tumbe 'A', Wingwi Kije na Maziwang'ombe na skuli moja ya ghorofa katika eneo la Mtopepo ipo katika hatua za awali. Aidha, ukamilishaji wa madarasa 237 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi unaendelea na uko katika hatua za umalizaji.
- iv) Serikali imeongeza idadi yaskuli za msingi zinazopatiwa huduma ya lishe kutoka skuli 42 na kufikia 50 ambapo wanafunzi 27,471 wanafaidika na mradi huo. Aidha, Serikali inawapatia huduma ya chakula wanafunzi wote 63,099 wa maandalizi wa skuli za Serikali.
- v) Wizara inaendelea kutoa ruzuku kwa Skuli zote za Maandalizi na Msingi za Serikali (262 za Maandalizi na 341 za Msingi).
- vi) Jumla ya walimu 889 wapya wamepangija kazi katika skuli za Maandalizi na Msingi Unguja na Pemba (416 Unguja na 473 Pemba).

- vii) Wizara kwa Kushirikiana na Taasisi ya Maisha Bora Foundation ya Mama Maryam Mwinyi imefanya uhamasishaji wa uandikishaji wanafunzi katika ngazi ya Elimu Maandalizi na Msingi.

Matokeo ya muda Mfupi

- i). Jumla ya wanafunzi 105,101 sawa na asilimia 82.5 wameandikishwa katika ngazi ya elimu ya maandalizi na wanafunzi 403,886 sawa na asilimia 103.8 wameandikishwa katika ngazi ya elimu ya msingi.
- ii). Jumla ya wanafunzi 58,678 wapya wameandikishwa darasa la kwanza kwa mwaka 2025, kati ya hao wanafunzi 52,136 sawa na asilimia 88.9 wamepitia elimu maandalizi. Jadweli namba 15C linatoa ufanuzi zaidi.
- iii). Jumla ya wanafunzi 46,021 sawa na asilimia 96.66 Wamefaulu mitihani yao ya kumaliza ngazi ya elimu ya msingi na kujiunga elimu ya sekondari.
- iv). Uwiano wa walimu kwa wanafunzi umeimarika kutoka 29 mwaka 2024 hadi kufikia 28 mwaka 2025 kwa ngazi ya elimu ya maandalizi na kutoka 42 mwaka 2024 hadi kufikia 39 mwaka 2025 kwa ngazi ya elimu msingi.
- v). Msongamano wa wanafunzi darasani umepungua kutoka uwiano wa wanafunzi 52 kwa darasa mwaka 2024 hadi kufikia 50 mwaka 2025 kwa ngazi ya elimu ya maandalizi na kutoka 60 hadi 42 kwa ngazi ya elimu ya msingi.
- vi). Jumla ya Skuli 237 za Msingi za Serikali sawa na asilimia 70 zinaendeshwa kwa mtindo wa shifti moja tu.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.

20. Mheshimiwa Spika, Programu hii inalenga kutoa na kuimarisha elimu ya Sekondari. Kwa mwaka 2024/25, Jumla ya **Tsh. 242,537,540,535** zimepangwa kutumika, kati ya fedha hizo **Tsh. 111,428,040,535** ni kwa ajili ya kazi za kawaida zikiwemo Tsh. **90,674,266,000** kwa ajili ya mishahara, **Tsh. 20,753,774,535** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Tsh. 131,109,500,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 142,639,189,633** sawa na asilimia 59 ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 76,672,985,672** sawa na asilimia **85** zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na **Tsh. 12,156,571,118** sawa na asilimia **59** zimetumika kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **Tsh. 53,809,632,843** sawa na asilimia **41** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 36,262,083,221** sawa na asilimia **40** ni kutoka SMZ na **Tsh. 17,547,549,622** sawa na asilimia **43** ni kutoka kwa wahisani. Fedha hizo zilitumika kutekeleza shughuli zifuatazo: -

- i. Jumla ya skuli za sekondari 193 (111 Unguja na 82 Pemba) zimepatiwa vifaa vya maabara na kemikali kwa ajili ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne mwaka 2024. Aidha, Wizara imenunua na kusambaza vifaa vya kujifunza na kufundishia kwa skuli saba zinazofundisha somo la uchoraji (Fine Art), skuli tatu zinazofundisha maarifa ya nyumbani na ushoni (home economy) na skuli sita zinazofundisha somo la Kompyuta. Pia, vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya masomo ya ufundi katika fani za Umeme, Ujenzi na Makenika vimenunuliwa na kusambazwa katika skuli za Ufundi Mikunguni na Kengeja.

- ii. Jumla ya skuli 23 zenyе kidato cha sita zimepatiwa vifaa vya maabara na kemikali kwa ajili ya mtihani wa Taifa. Aidha, Skuli ya Haile Selasie imepatiwa vifaa kwa ajili ya somo la michezo (Physical Education), skuli ya Benbella imepatiwa vifaa vya somo la Nutrition. Vifaa vyote hivyo vimesambazwa kwa watahiniwa wa mtihani wa kidato cha sita uliofanyika mwezi Mei 2025.
- iii. Wizara inaendelea kutoa ruzuku za uendeshaji kwa skuli 225 za Sekondari Unguja na Pemba, ambapo jumla ya Tsh. 1,994,572,744 zimetumika. Vilevile, kiasi cha Tsh. 165,000,240 zimetumika kwa ajili ya ruzuku za uendeshaji wa vituo 22 vya ubunifu wa kisayansi (Hubs) Unguja na Pemba.
- iv. Ujenzi wa skuli 14 za Sekondari za chini unaendelea katika maeneo ya Kama, Mwenge, Chuini, Mbuzini, Kisauni, Tunguu, Koani, Karume, Kinowe, Sizini, Simai, Finya, Vikunguni na Furaha. Aidha, Jumla ya dakhalia 14 zinaendelea na ujenzi katika skuli ya Lumumba, Mikindani, Misufini, Donge sekondari, Paje Mtule, Hasnuu Makame, Kiwani, Fidel Castro, Chwaka Tumbe na Maziwa Ng'ombe.
- v. Ujenzi wa skuli tisa za ghorofa unaendelea. Skuli nane kati ya hizo upo katika hatua za ukamilishwaji katika maeneo ya Regeza Mwendo, Mfenesini, Maungani, Chukwani, Muungano, Kifundi, Gamba na Makunduchi. Aidha, Skuli moja katika eneo la Vitongoji ipo katika hatua ya msingi.
- vi. Wizara inaendelea na ujenzi wa madarasa mapya 291 Unguja na Pemba. Aidha, jumla ya madarasa 79 yalianzishwa na nguvu za wananchi yanaendelea kwa

- hatua ya ukamilishwaji na jumla ya skuli 34 zinaendelea na ukarabati Unguja na Pemba.
- vii. Serikali inaendelea kutoa huduma za dakhalia zikiwemo za chakula katika skuli 21 za Serikali Unguja na Pemba. Jumla ya wanafunzi 6,395 wanafaidika na huduma hizo.
 - viii. Wizara imefanya warsha mbalimbali kwa walimu wakuu, wasaidizi na walimu wa masomo juu ya uelewa wa mtaala mpya wa umahiri kwa Unguja na Pemba.
 - ix. Jumla ya wanafunzi 40 wa kike na walimu watano wameshiriki katika mafunzo ya TEHAMA na watendaji 10 wa Idara ya Elimu ya Sekondari wameshiriki mafunzo ya muda mfupi ya TEHAMA katika Chuo cha Serengeti East Afrika Management Consultant kilichopo Dar es salaam.
 - x. Jumla ya skuli 32 za Sekondari zimeanza kufundisha masomo ya Amali kuzingatia utekelezaji wa Mtaala mpya.
 - xi. Jumla ya wanafunzi 1,479 ambao hawakufanya vizuri katika Mtihani wa kidato cha Nne wameandikishwa na wanapatiwa mafunzo ya masomo ya Amali katika vituo vya mafunzo ya Amali.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Jumla ya wanafunzi 129,583 kati yao wanawake 70,574 na wanaume 59,009 wameandikishwa katika ngazi ya Elimu ya Sekondari ya awali (kidato 1 – 4). jadweli namba 16B linatoa ufanuzi.
- ii. Asilimia ya uandikishaji imeongezeka kutoka asilimia 63.8 mwaka 2024 hadi kufikia asilimia 68.2 mwaka wa 2025.

- iii. Wastani wa Uwiano wa wanafunzi kwa darasa ngazi ya Sekondari umeimarika na kufikia 41 mwaka 2025 ikilinganishwa na shabaha ya wanafunzi 45 kwa darasa.
- iv. Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu ngazi ya elimu ya Sekondari umefikia wanafunzi 21 kwa mwalimu mwaka 2025. jadweli namba 45 (A) ii) linatoa ufanuzi.
- v. Jumla ya wanafunzi 18,934 (wanaume 8,905 na wanawake 10,029) sawa na asilimia 84.44 wamefaulu Mtihani wa kidato cha pili na kuendelea na masomo ya Kidato cha Tatu. Jadweli namba 35 linatoa ufanuzi.
- vi. Jumla ya wanafunzi 26,017 walifanya mtihani wa kidato cha nne Novemba 2024, wanafunzi 21,338 sawa na asilimia 82 wamefaulu mtihani huo. Kati ya hao, wanafunzi 7,914 sawa na asilimia 37 wataendelea na masomo ya kidato cha tano katika skuli mbali mbali kwa Unguja na Pemba.
- vii. Jumla ya Skuli 184 za Sekondari za Serikali sawa na asilimia 81 zinaendeshwa kwa mtindo wa shifti moja tu.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

21. Mheshimiwa Spika, Madhumuni ya programu ya Elimu ya Juu ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujiajiri au kuajiriwa. Programu hii ina programu ndogo moja ya mafunzo ya ualimu na maeneo matano ya huduma, ikiwemo Huduma ya Ushauri na Utafiti; Huduma ya Sayansi na Teknolojia, Huduma ya Teknolojia – IIT Madras, Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu. Programu hii ilipangisha kutumia

jumla ya **Tsh. 210,747,937,698**. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 35,981,775,968** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na **Tsh. 174,766,162,000** kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 66,523,956,023** sawa na asilimia **32** ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 23,445,724,211** sawa na asilimia **78** zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na **Tsh. 1,183,468,178** sawa na asilimia 21 zimetumika kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **Tsh. 41,894,763,634** sawa na asilimia **24** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 20,272,855,686** sawa na asilimia **25** ni kutoka SMZ na **Tsh. 21,621,907,948** sawa na asilimia **23** ni kutoka kwa wahisani.

Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu

- 22. Mheshimiwa Spika**, Madhumuni makubwa ya Programu hii ni kuwawezesha walimu kuwa wabunifu, wataalamu na wenye uwezo wa kuongoza ili kukuza ubora wa elimu. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mafunzo ya Ualimu. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya **Tsh. 19,442,859,698**. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 905,691,698** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Tsh. 3,030,084,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Tsh. 15,507,084,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 2,152,535,540** sawa na asilimia **11** ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 1,894,077,300** sawa na asilimia **63** zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na **Tsh. 99,028,215** sawa na asilimia **11** zimetumika kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **Tsh. 159,430,025** sawa na asilimia **2** zilipatikana kutoka kwa

wahisani. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama hivi ifuatavyo: -

- i. Wizara imeanza kutoa mafunzo ya muongozo wa kuendesha mafunzo kazini katika ngazi ya Skuli (SBI). Jumla ya walimu 1,933 walishiriki mafunzo hayo wakiwemo washauri wa masomo 33, walimu wakuu na wasaidizi 1,029, wakuu wa masomo 495 na walimu watakwimu 376. Mafunzo hayo yalifanyika kwa skuli 156 za majoribio kutoka Wilaya ya Kusini na Magharibi 'A' kwa Unguja na Wilaya ya Wete kwa Pemba.
- ii. Wizara imefanya ziara 773 za ufuatiliaji wa shughuli za ufundishaji na utekelezaji wa mafunzo mbalimbali yanayotolewa kwa walimu kwa Unguja na Pemba.
- iii. Jumla ya waratibu na washauri 113 wa masomo ya maandalizi, msingi na sekondari kutoka vituo vyta walimu Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya mbinu za ufuatiliaji na tathmini.
- iv. Wizara inaendelea na Utaratibu wa kukirejesha Chuo cha Ualimu Nkrumah. Chuo kitafunguliwa katika Skuli mpya iliyopo Mfenesini hadi ujenzi wa Chuo kipyaa unaotarajiwa kuanza mwaka 2026 katika eneo la Dole utakapokamilika.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Jumla ya wanafunzi 1,090 wamejiunga na vyuo vyta ualimu vyta Mazizini Unguja na Kiuyu Pemba mwaka 2024.
- ii. Jumla ya wahitimu 1,290 wakiwemo 606 ngazi astashahada na 684 ngazi ya stashahada wamehitimu mafunzo ya Ualimu mwaka 2024 katika vyuo vyta ualimu Mazizini Unguja na Kiuyu Pemba.

- iii. Programu za mafunzo ya Ualimu zimeongezeka kutoka programu saba mwaka 2023 hadi programu nane mwaka 2024.
- iv. Jumla ya walimu 3,028 wakiwemo wanaume 1,008 na wanawake 2020 wamepatiwa mafunzo kazini (walimu 1,888 Unguja na 1,140 Pemba).
- v. Jumla ya walimu wapya 500 (wanaume 296 na wanawake 204) wamepatiwa mafunzo kazini kuhusu ufaraguzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, matumizi ya TEHAMA, matayarisho ya madaftari manne ya kazi pamoja na mafunzo ya nidhamu Mbadala.

Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti

- 23. Mheshimiwa Spika**, Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti ina lengo la kuwaandaa wanafunzi kuingia katika fani za kitaalamu na ajira.
- 24. Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kilitengewa jumla ya **Tsh. 110,302,312,000** zikiwemo ruzuku ya **Tsh. 19,568,400,000** kwa ajili ya mishahara na **Tsh. 90,733,912,000** ni kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 26,505,309,819** sawa na asilimia **24** ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 15,461,030,958** sawa na asilimia **79** zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na **Tsh. 11,044,278,861** Kwa upande wa fedha za maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 155,000,000** sawa na asilimia **1** ni kutoka SMZ na **Tsh. 10,889,278,861** sawa na asilimia **17** ni kutoka kwa wahisani Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Jumla ya wanafunzi wapya 2,326 (wanaume 1,036 na wanawake 1,290) wamedahiliwa kujiunga na masomo katika ngazi mbalimbali. Aidha, chuo kimefanya mahafali ya 20 kwa wahitimu ambapo jumla ya wahitimu 2,291 (wanaume 886 na wanawake 1,405) wametunukiwa vyeti wakiwemo wahitimu watano wa uzamivu, 69 wa uzamili, 789 wa shahada, 930 wa stashahada na 498 wa astashahada.
- ii. Chuo kimewalipia ada za masomo ya muda mrefu wafanyakazi wake 28 (wanaume 13 na wanawake 15) kwa fani mbalimbali za kipaumbele kuititia mradi wa HEET katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu wafanyakazi watano, Shahada ya Uzamili 19, Shahada ya kwanza wanenye. Aidha, wafanyakazi 13 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ya Mpango Mkakati na Usimamizi wa rasilimali watu, uhudumu, Usimamizi wa mali na bidhaa katika Uhasibu na uandaaji wa bajeti.
- iii. Kongamano la siku ya utafiti limefanyika likiwa na lengo la kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika elimu, kuendeleza programu za mafunzo endelevu kwa walimu na watafiti na matumizi ya matokeo ya utafiti katika utayarishaji wa sera bora za elimu. Kongamano hilo lilifunguliwa na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdulla ambalo limejumuisha washiriki 500 wakiwemo wasomi, watunga sera, wadau wa elimu kutoka ndani na nje ya nchi.
- iv. Mapitio ya Mitaala ya programu za Shahada ya Sayansi ya kompyuta (BSc Computer science), Sayansi ya Kilimo Jumuishi (BSc in Agriculture General), Doctor of Medicine (MD) na Doctor of Dental Surgery

(DDS) yamekamilika na kuwasilishwa TCU kwa kuthibitishwa. Mitaala ya programu tatu ikiwemo Bachelor of Information Technology Application and Management (BITAM), BSc.in Biomedical Engineering na MSc. Chemistry imepitishwa na Wizara ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia, hatua inayofuata ni kuwasilishwa SENET na TCU. Aidha, tathmini ya mahitaji (Need assessment) ya kuandaa mtaala mpya wa programu ya BSc in Aquatic and Fisheries Sciences imefanyika.

- v. Kazi ya uandaaji wa michoro ya ujenzi wa Skuli ya Afya na Sayansi ya Tiba na Skuli ya Meno na Klinik yake imekamilika. Taratibu za kumpata mzabuni kwa ajili ya ujenzi zinaendelea. Aidha, utiaji saini wa mkataba wa ujenzi wa Dakhalia ya wanawake umefanyika tarehe 19/02/2025 baina ya SUZA na Kampuni ya Emirate Construction Limited na ujenzi umeanza.
- vi. Wizara inaendelea na ujenzi wa jengo la Skuli ya Kilimo na Maabara ambapo ujenzi wa msingi tayari umekamilika. Aidha, Tathmini ya kumtafuta mshauri elekezi wa kutayarisha michoro na usimamizi wa ujenzi wa skuli ya elimu, nyumba za wafanyakazi, kituo cha wanafunzi na kiwanja cha michezo kwa hatua ya pili (technical evaluation) zimekamilika na tayari zimeshawasilishwa BADEA kwa ajili ya kuendelea na taratibu zinazofuata.
- vii. Wizara imefanya uzinduzi wa Mfumo mpya wa masomo ya kimtandao “My loft-My library of finger print” ambao utasaidia upatikanaji wa taarifa za kimasomo kwa njia rahisi. Aidha, ununuzi wa vifaa vya TEHAMA vikiwemo Kompyuta ‘desktop 110, Laptop

10 na CCTV 35' umefanyika na vifaa hivyo vimegaiwa katika kampasi zote za chuo.

- viii. Jumla ya Wanafunzi watatu wa Chuo kikuu cha Taifa wameibuka kuwa washindi katika shindano la Mawazo ya Kibiashara (Business Ideas) chini ya mradi wa Youth Ignite unaosimamiwa na Start hub Africa unaofadhiliwa na UNDP. Shindano hilo limeshirikisha wanafunzi 30 kutoka vyuo 10 nchini Tanzania.

Matokeo ya muda Mfupi

- i. Idadi ya Wanafunzi wanaomaliza ngazi mbalimbali za uzamivu, uzamili, shahada, stashahada na astashahada imeongezeka kutoka 2,102 mwaka 2024 hadi kufikia 2,291 mwaka 2025.
- ii. Jumla ya wanafunzi wapya 2, 326 (wanaume 1,036 na wanawake 1,290) wamedahiliwa kuijunga na masomo katika ngazi mbali mbali.
- iii. Jumla ya programu mpya tano zimeanzishwa katika ngazi ya Shahada ya Kwaza.
- iv. Jumla ya tafiti 12 zimefanyika na tafiti nane zinaendelea.

Huduma ya Sayansi na Teknolojia

- 25. Mheshimiwa Spika**, huduma ya Sayansi na Teknolojia ni miongoni mwa huduma muhimu katika kuinua kiwango cha Elimu ya Uhandisi, Sayansi na Teknolojia na kuimarisha maendeleo ya uchumi wa nchi. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Kwa mwaka 2024/2025, Taasisi hii ilitengewa ruzuku ya **Tsh. 36,749,866,000**. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 3,224,700,000** ni ruzuku kwa ajili ya mishahara na **Tsh. 33,525,166,000** ni kwa ajili ya kazi za Maendeleo. Hadi

kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 13,304,131,742** sawa na asilimia 36 ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 2,730,932,680** sawa na asilimia 85 zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi. Kwa upande wa fedha za Maendeleo, **Tsh. 10,573,199,062** sawa na asilimia **53** zilipatikana kutoka kwa wahisani. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo:

- i. Jumla ya wafanyakazi 34 wa Taasisi wanaendelea na masomo ya muda mrefu katika ngazi mbalimbali za masomo zikiwemo Shahada ya Uzamivu (PhD) 13, Shahada ya Uzamili 16, Shahada ya kwanza watatu na Astashahada wawili. Aidha, wafanyakazi 55 (wanawake 23 na wanaume 32) wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya muda mfupi kwa lengo la kuwaongezea uzoefu na ujuzi katika kazi.
- ii. Wizara imeingia makubaliano ya mashirikiano na Vyuo na Taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kukuza na kuendeleza fani ya sayansi na teknolojia hapa nchini. Mionganini mwa Taasisi za nje ni AP University (Belgium), Nanjing University of Aeronautics and Astronomy (China), Beijing Institute of Technology (BIT) (China), University of Liverpool (UK), Sapienza University (Italy), University of Cyprus, Puma Energy, GFP International (US), IDOM (Spain) na VACE (Austria). Kwa upande wa taasisi za ndani ya nchi. Wizara imefanya makubaliano na Arusha Technical College (ATC), National Institute of Transportation (NIT), VETA na Mnazi Mmoja Hospital. Kupitia mashirikiano hayo wafanyakazi na wanafunzi wamekua wakifaidika kukuza ujuzi wao katika nyanja mbalimbali.

- iii. Jumla ya wanafunzi wapya 914 (wanaume 702 na wanawake 212) wamesajiliwa kujiunga na fani mbalimbali. Kati ya hao, Shahada ya kwanza 102 (wanaume 73 na wanawake 29), Stashahada 416 (wanaume 260 na wanawake 156), Astashahada ni 396 (wanaume 369 na wanawake 27).
- iv. Jumla ya wanafunzi 3,457 wakiwemo wanawake 942 na wanaume 2,515 wanaendelea na masomo katika fani mbalimbali. Jadweli 30 (d) linatoa ufanuzi zaidi.

Matokeo ya muda Mfupi

- i. Jumla ya wanafunzi 739 (wanawake 288 na wanaume 451) wamedahiliwa katika ngazi na fani mbali mbali zinazotolewa na Taasisi.
- ii. Jumla ya wanafunzi 940 (wanaume 681 na wanawake 259) wamehitimu masomo yao katika ngazi za Shahada (31), Stashahada (201) na Astashahada (708) wanafunzi wote hawa wametunukiwa vyeti vyao.

Huduma ya Teknolojia – IIT Madras

- 26. Mheshimiwa Spika, Huduma ya Teknolojia – IIT Madras** ina lengo la kuwaandaa wanafunzi katika elimu ya Sayansi na Teknolojia kuingia katika fani za kitaalamu na ajira. Huduma hii inatolewa katika Taasisi ya Teknolojia ya India. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Jumla ya **Tsh. 12,600,000,000** zilipangwa kutumika, kati ya fedha hizo **Tsh. 2,600,000,000** ni kwa ajili ya matumizi ya mengineyo na **Tsh. 10,000,000,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 2,463,845,686** sawa na asilimia **20** ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 380,990,000** sawa na asilimia **15** zimetumika kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya

Tsh. 2,082,855,686 sawa na asilimia 21 zilipatikana kutoka SMZ. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo:

- i. Jumla yawanafunzi wapya 61 (wanaume 43 na wanawake 18) wamedahiliwa kujiunga na masomo katika ngazi ya Shahada ya kwanza na Shahada ya uzamili (40 shahada ya kwanza na 21 shahada ya uzamili).
- ii. Jumla ya fani mbili zinaendelea kutolewa zikiwemo “Data Science and Artificial Intelligence” na “Ocean Structure”
- iii. Ujenzi wa utanuzi wa Chuo cha IITM unaendelea katika hatua ya ujenzi wa dakhalia.
- iv. Jumla ya wanafunzi saba wa Chuo cha IIT Madras (wanaume wanne na wanawake watatu) wamepatiwa ufadhili wa masomo katika ngazi ya shahada ya kwanza na shirika la Airtel.

Matokeo ya Muda Mfupi

Uandikishaji wa wanafunzi katika taasisi umefikia jumla ya wanafunzi 104 wakiwemo 30 wanawake na 74 wanaume kutoka katika mataifa mbali mbali yakiwemo India (56), Tanzania (40), Nepal (01), Zambia (06) na Kenya (01).

Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu

27. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar inatekeleza majukumu makuu matatu, ambayo ni kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji wenye sifa za kujiunga na masomo ya elimu ya juu; kusimamia na kufuutilia nafasi za ufadhili wa masomo kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo ndani na nje ya Tanzania na kukusanya marejesho ya mikopo ya wanafunzi kutoka kwa wanufaika wote.

28. **Mheshimiwa Spika, Kwamwakawafedha 2024/2025, jumla ya Tsh. 27,865,100,000** zimetengwa kutekeleza shughuli za huduma hii. Kati ya fedha hizo **Tsh. 2,865,100,000** kwa ajili ruzuku ya kazi za kawaida ikiwemo **Tsh. 754,500,000** za mishahara, **Tsh. 2,110,600,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Tsh. 25,000,000,000** za maendeleo zilitengwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wapya na wanaoendelea na masomo ya Elimu ya Juu. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 19,335,251,822** sawa na asilimia 69 ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 641,918,527** sawa na asilimia **85** zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na **Tsh. 658,333,295** sawa na asilimia **31** zimetumika kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **Tsh. 18,035,000,000** sawa na asilimia **72** kutoka SMZ zilipatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Jumla ya wanafunzi 11,495 wapya na wanaonDELETEA na masomo ya elimu ya juu (4,484 wanaume na 7,011 wanawake) wamepatiwa mikopo ya elimu ya juu wakiwemo wanafunzi wapya 7,198 na 4,297 wanaoendelea na masomo
- ii. Jumla ya wanafunzi 197 wakiwemo wapya 60 na 137 wanaoendelea na masomo wamefaidika na ufadhili wa masomo kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni motisha kwa wanafunzi waliofaulu vizuri zaidi kwa daraja la kwanza katika mitihani ya Taifa ya Kidato cha Sita katika masomo ya Sayansi, Biashara na Sanaa.
- iii. Jumla ya wanafunzi wapya 60 wamepatiwa ufadhili wa masomo kwa vyuo vya ndani ya nchi wakiwemo 27 wa Chuo Kikuu cha Zanzibar kilichopo Tunguu kupitia ufadhili wa taasisi za Darul Iman, wanafunzi 33 wa

Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait cha Chukwani walipatiwa ufadhili kupitia Shirika la “Direct Aid” na wanafunzi 8 wamepatiwa ufadhili wa masomo kutoka NAMA Foundation.

Matokeo ya muda Mfupi

- i. Idadi ya wanafunzi wapya waliopatiwa mikopo ya elimu ya juu imeongezeka kutoka wanafunzi 2,502 mwaka 2023/2024 hadi kufikia wanafunzi 7,198 kwa mwaka 2024/2025, sawa na asilimia 74 ya wanafunzi 9,758 waliomba mikopo.
- ii. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla Tsh 3.43 bilioni zimekusanywa sawa na asilimia 62 ya lengo lililowekwa.
- iii. Idadi ya wanafunzi 197 wamepewa ufadhili wa masomo wa SMZ mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 18 ukilinganisha na matarajio ya wanafunzi 167.

Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu

- 29. Mheshimiwa Spika**, huduma hii ina jukumu la kusimamia na kutathmini maendeleo ya elimu ya juu na inatekelezwa na Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kitengo kilitengewa jumla ya **Tsh. 145,000,000** kutoka Serikalini kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 49,080,000** sawa na asilimia **34** zimepatikana. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo: -
- i. Wizara imefanya ufuatiliaji na tathmini katika vyuo vikuu 3 na vyuo vya kati 21 kuangalia utoaji wa Elimu na uendeshaji katika Taasisi hizo pamoja na kusikiliza na kutatua changamoto mbalimbali za wanafunzi wanazokutana nazo Vyuoni.

- ii. Wizara imefanya Maonesho ya 5 ya Wiki ya Elimu ya Juu katika Viwanja vya Maisara mwezi wa Julai, 2024 kwa Lengo la kutoa Elimu na miongozo kwa wadau wote wa Elimu pamoja na wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita ambao wanatarajiwa kujiunga na Elimu ya Juu. Jumla ya Taasisi 77 zilishiriki na zimepata fursa ya kuonesha kazi zao. Pia, wadau 26,227 katи ya hao wanaume 12,036 na wanawake 14,191 walitembelea katika mabanda ya maonesho hayo.
- iii. Jumla ya Viongozi 26 wa Serikali za wanafunzi na wakuu wa vyuo 11 wameshiriki katika Program za uhamasishaji juu ya kupunguza masuala ya Udhailishaji katika Taasisi za Elimu pamoja na jamii. Aidha, wanafunzi 3,566 (Wanawake 1,886 na Wanaume 1,680) katika skuli 37 wamepatiwa elimu na miongozo juu ya kuchagua fani zinazoendana na mahitaji.
- iv. Wizara imetangaza nafasi za masomo za ndani na nje ya nchi ya Tanzania kwa viwango vya Shahada ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu katika fani mbalimbali zikiwemo; Udaktari, Uchumi, Ukandarasi, Ualimu, Uuguzi, Sayansi ya Mazingira, Kilimo, Usimamizi wa Biashara na Utawala, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Maendeleo ya Jamii, na Sayansi ya TEHAMA. Nafasi za masomo zilizotangazwa kwa mwaka 2024/2025 ni kutoka nchi wahisani 17 zikiwemo nchi ya Algeria, Jumuiya ya Madola, Brunei, Hungary, China, Mauritius, Misri, Indonesia, Saudi Arabia, Muslim Communities in non - member Countries, Pan Africa University, Azerbaijan, Australia, German, Russia, Kemitraan Negara Berkembang na Uturuki.

- v. Jumla ya waombaji 206 (wanaume 89 na wanawake 117) waliwasilisha maombi ya nafasi za ufadhilli wa masomo nje ya nchi kwa mwaka 2024/2025, Nchi ambazo zimetoa majibu ya waliofanikiwa kupata nafasi za ufadhilli ni China, Algeria, Misri na uturuki, ambapo wanafunzi waliopata nafasi katika ufadhilli wa China ni wanafunzi 9 (wanaume 5 na wanawake 4), Algeria wanafunzi 21 (wanaume 10 na wanawake 11), Misri mwanamke 1, na Uturuki wanawake 22, Wizara inasubiri majibu ya Nchi nyengine zilizotoa ufadhilli wa masomo.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Jumla ya wanafunzi 12,700 wanaendelea na masomo ya Elimu ya Juu katika vyuo vikuu vitatu vya Zanzibar wakiwemo wanawake 7,829 na wanaume 4,871. Aidha, jumla ya wanafunzi 9,727 wakiwemo wanawake 6,482 na wanaume 3,245 wanaendelea na masomo katika vyuo vya kati.
- ii. Jumla ya wanafunzi 250 (125 wanawake na 125 wanaume) wamepata udhamini wa elimu ya juu ndani na nje ya nchi, wanafunzi 53 wamedhaminiwa na Nchi za nje na wanafunzi 197 wamedhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

- 30. Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kuwajengea uwezo vijana katika ushindani wa soko la ajira kwa kuwapatia mafunzo mbadala na amali. Programu hii ina programu ndogo mbili; Mafunzo ya Amali na Elimu Mbadala na Watu Wazima. Programu ilitengewa jumla ya **Tsh. 41,002,809,755**. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 11,502,809,755** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida ikiwemo **Tsh. 5,183,253,000** kwa ajili ya malipo

ya mishahara, **Tsh. 6,319,556,755** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Tsh. 29,500,000,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 8,843,435,637** sawa na asilimia **22** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 7,494,820,734** sawa na asilimia 65 ni fedha za Matumizi ya kawaida ikiwemo **Tsh. 4,420,502,683** sawa na asilimia **85** kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Tsh. 3,074,318,051** sawa na asilimia **49** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Tsh. 1,348,614,903** sawa na asilimia 5 ni kwa ajili ya Maendeleo kutoka kwa wahisani. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima

31. Mheshimiwa Spika, programu hii inatekelezwa na Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima na ina lengo la kupunguza kiwango cha wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wanajamii. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, programu hii ilitengewa jumla ya **Tsh. 3,404,809,755**. Kati ya fedha hizo **Tsh. 1,391,753,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Tsh. 2,013,056,755** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 1,315,126,107** sawa na asilimia **39** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 233,438,735** sawa na asilimia **12** ni fedha za Matumizi mengineyo na **Tsh. 1,081,687,372** sawa na asilimia **78** ni kwa ajili ya Mishahara. Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Jumla ya wanafunzi 1,902 wakiwemo wanaume 1,171 na wanawake 731 wamesajiliwa kuijunga na madarasa 97 ya Elimu Mbadala Unguja na Pemba.
- ii. Jumla ya wanakisomo 7,011 sawa na asilimia 90 wa kisomo cha Watu Wazima wamepimwa katika

hatua zote nne za kisomo. Kati yao, 3,950 sawa na asilimia 63 wamefaulu na 391 sawa na asilimia 73 wamekombolewa.

- iii. Jumla ya walimu wa madarasa ya kisomo na wakuu wa vituo 319 wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusu upimaji wa wanafunzi. Aidha, jumla ya madarasa 23 ya wanakisomo yamefanyiwa ukaguzi kutathmini ubora wa mafunzo yanayotolewa
- iv. Wizara imefanya maadhisho ya wiki ya elimu ya Watu wazima kwa lengo la kuhamasisha wananchi kujiunga katika madarasa ya kisomo na vituo vya elimu Mbadala.
- v. Wizara inaendelea na kazi ya tathmini ya programu zinazoendeshwa na Idara ya elimu Mbadala na Watu Wazima kwa lengo la kuboresha programu zilizopo na kuanzisha programu mpya zinazoendana na mahitaji ya soko la ajira.
- vi. Wizara inaendelea kuwajengea uwezo vijana katika fani mbalimbali ambapo vijana 150 (75 Unguja na 75 Pemba) wamepatiwa mafunzo ya ushoni, vijana 42 wakiwemo wanaume 35 na wanawake saba wamepatiwa mafunzo ya uchongaji wa samani pamoja na ukarabati wa madawati yaliyoharibika. Aidha, vijana 150 (75 Unguja na 75 Pemba) wanaendelea na mafunzo ya Lughaa, ushoni, upishi na upambaji wa hina na piko na uchongaji katika Vituo vya Wingwi, Rahaleo na Mwerapongwe.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Jumla ya wanafunzi 1,902 wakiwemo wanaume 1,171 na wanawake 731 wenye umri kati ya miaka 7 hadi 14 waliokuwa nje ya skuli wamerejeshwa skuli Unguja na Pemba.

- ii. Jumla ya wanakisomo 7,053 wakiwemo wanaume 694 na wanawake 6,359 wameandikishwa katika madarasa ya kisomo kwa Unguja na Pemba.

Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali

- 32. Mheshimiwa Spika**, Programu hii ndogo ilitengewa jumla ya Tsh. **37,598,000,000**. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 8,098,000,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida ikiwemo Tsh. **3,791,500,000** kwa ajili ya malipo ya mishahara, **Tsh. 4,306,500,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Tsh. 29,500,000,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 7,528,309,530** sawa na asilimia **20** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 3,338,815,311** sawa na asilimia 88 ni fedha za Matumizi ya Mshahara na **Tsh. 2,840,879,316** sawa na asilimia **66** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na **Tsh. 1,348,614,903** sawa na asilimia 5 ni kwa ajili ya kazi za Maendeleo. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo: -
- i. Ujenzi wa Kituo cha Afya katika Chuo cha Amali Mkokotoni unaendelea kwa hatua ya uezekaji. Aidha, Wizara imefanya ukarabati wa majengo mbali mbali ya vyuo vya amali Mkokotoni Unguja na Vitongoji Pemba hasa katika ujenzi wa njia za watu wenye mahitaji maalum (ramps) na jiko.
 - ii. Wizara imeandaa Muongozo wa kamati ya ushauri ya vyuo, rasimu ya mkataba wa ukaguzi wa ndani, rasimu ya Sera ya viashiria hatarishi na Sera ya mafunzo. Miongozo hii imewasilishwa kwa wadau kwa ajili ya maoni Unguja na Pemba.
 - iii. Wizara imenunua na kusambaza vifaa mbalimbali vya kujifunzia na kufundishia katika vyuo vitano vya

Mamlaka ya mafunzo ya Amali kwa ajili ya mtihani wa Taifa, miongoni mwa vifaa hivyo ni vitambaa, mbao, waya, rangi na vyuma.

- iv. Jumla ya vituo vipyta 12 (sita Unguja na sita Pemba) vimepatiwa usajili wa muda baada ya kukidhi vigezo. Aidha, vyuo saba vimemaliza usajili wao wa miaka miwili na kusajiliwa upya kwa ajili ya kuendelea kutoa mafunzo. Pia Jumla ya walimu watano wamepatiwa leseni za kufundishia mafunzo ya amali.
- v. Wizara imefanya ufuatiliaji na ukaguzi wa vyuo 34 vinavyotoa mafunzo ya amali kwa Unguja na Pemba, lengo ni kutathmini ubora wa mafunzo yanayotolewa na changamoto zinazojitokeza katika ufundishaji. Aidha, Wizara ilifanya ukaguzi kwa wakufunzi wa vyuo vitano vyta Mafunzo ya Amali uliohusisha mawanda (scope) ya zana za ufundishaji. Wakufunzi waliokaguliwa ni kutoka Chuo cha Amali Mkokotoni, Mwanakwerekwe na Makunduchi kwa Unguja, Vitongoji na Daya kwa upande wa Pemba.
- vi. Jumla ya wakufunzi 22 kutoka vyuo vitano vyta Mafunzo ya Amali wamepatiwa mafunzo ya kimbinu na kiujuzi (pedagogical technical) na 52 wamepatiwa mafunzo ya uelewa wa matumizi ya multimedia katika kufundishia. Pia wakufunzi 65 wamepatiwa mafunzo ya zana za ufundishaji (logbook) kwa Unguja na Pemba. Aidha, Wafanyakazi 21 wanaendelea na masomo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi na wafanyakazi 57 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali zikiwemo ‘water treatment; Standalone solar system; small boat handling na aluminium work’.

vii. Taratibu za Ujenzi wa vyuo vitano vya Mafunzo ya Amali kupitia mradi wa SEBEP zinaendelea, kazi ya kuandaa michoro imekamilika. Vyuo hivyo vitajengwa katika maeneo ya Bweleo, Pangatupu na Jendele kwa Unguja Tumbe Mashariki na Chambani kwa Pemba.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Idadi ya vijana waliojiajiri katika vikundi vya wahitimu wa Mafunzo ya Amali ambao wamepatiwa mikopo imeongezeka kutoka vikundi 28 mwaka 2024 hadi kufikia vikundi 32 mwaka 2025.
- ii. Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Mafunzo ya Amali imeongezeka kutoka wanafunzi 2,217 mwaka 2024 hadi kufikia wanafunzi 2,644 mwaka 2025.
- iii. Idadi ya wahitimu wa Mafunzo ya Amali imeongezeka kutoka wahitimu 860 mwaka 2023/2024 hadi kufikia wahitimu 1,595 mwaka 2024/2025.

PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU

- 33. Mheshimiwa Spika**, programu hii ina lengo la kuhakikisha elimu inayotolewa katika ngazi zote ni yenye ubora unaokidhi mahitaji ya mwenye kuhitimu, jamii na taifa kwa ujumla. Programu hii ilitengewa jumla ya **Tsh. 48,565,662,396**, Kati ya fedha hizo, **Tsh. 7,313,183,396** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Tsh. 7,607,479,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Tsh. 33,645,000,000** ni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 20,259,402,114** sawa na asilimia **42** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 5,811,195,614** sawa na asilimia **80** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Tsh. 6,782,402,218** sawa na asilimia **89** ni kwa ajili ya mishahara na **Tsh. 7,665,804,282** sawa na asilimia **23** ni kwa kazi za Maendeleo ambapo **Tsh. 83,731,250** sawa na asilimia **0.4** kutoka SMZ na **Tsh.**

7,582,073,032 sawa na asilimia **51** kutoka kwa wahisani. Progamu hii ina jumla ya programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama ifuatavyo: -

Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia

34. Mheshimiwa Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu na kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za elimu ya maandalizi, msingi, Sekondari na mafunzo ya Ualimu. Shughuli za utoaji wa huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Elimu Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Taasisi ilitengewa ruzuku yenye jumla ya **Tsh. 12,598,600,000**, kati ya fedha hizo, **Tsh. 1,853,600,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida zikiwemo **Tsh. 1,423,900,000** za mishahara na **Tsh. 429,700,000** kwa matumizi mengineyo. Aidha, **Tsh. 10,745,000,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2025, jumla ya **Tsh. 3,022,022,402** sawa na asilimia 24 zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 1,166,438,121** sawa na asilimia 82 ni fedha za Matumizi ya Mshahara, **Tsh. 189,780,000** ni kwa ajili ya matumizi ya mengineyo na **Tsh. 1,665,804,282** sawa na asilimia 16 ni kwa ajili ya Maendeleo ambapo **Tsh. 83,731,250** sawa na asilimia 4 kutoka SMZ na **Tsh. 1,582,073,032** Wahisani sawa na asilimia **18**. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Wizara imetayarisha mtaala mpya wa Stashahada ya Mafunzo ya Ualimu ngazi ya elimu ya Maandalizi, Msingi na Elimu Mjumuisho. Aidha, Mtaala huo unatarajiwa kuanza kutumika rasmi mwezi wa Julai 2025.
- ii. Wizara imetayarisha Moduli 12 za kufundishia mafunzo ya ualimu. Moduli saba (7) za ngazi ya Sekondari kwa masomo ya Hisabati, Baiolojia, Kemia, Fizikia, Kiingereza na TEHAMA katika kufundishia na moduli tano za ngazi ya Msingi kwa masomo

ya Sayansi, Kiingereza, Hisabati na TEHAMA katika kufundishia kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa Mitaala mipyä.

- iii. Wizara imetoa mafunzo kwa walimu juu ya matumizi ya mtaala mpyä wa umahiri ambapo walimu 5,879 wa skuli za Serikali na binafsi walipatiwa mafunzo hayo.
- iv. Jumla ya vitabu 10 vya ngazi (level reader) vimeandaliwa kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa wanafunzi kwa stadi za kusoma kuandika na kuhesabu katika skuli za msingi. Vitabu viwili vya somo la Kiswahili, viwili vya Kiingereza, viwili vya Hisabati, viwili vya Sanaa za Ubunifu na Michezo, kimoja cha Sayansi na Teknolojia na kimoja cha Sayansi Jamii.
- v. Wizara imeandaa miongozo ya kujifunzia na kufundishia wanafunzi wenyewe ulemavu wa akili, ulemavu wa kuona na kusikia. Aidha, miongozo ya kuandika na kufanya tathmini ya ubora wa vitabu na vifaa vyengine vya kufundishia vikiwemo vifaa vya kielektroniki imeimariswa.
- vi. Wizara inaendelea na matayarisho ya mifumo ya upimaji na tathmini (National Assessment Framework and Large Scale Assessment) kwa ajili ya utekelezaji wa mtaala mpyä wa umahiri.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Mitaala mitatu mipyä ya mafunzo ya Ualimu kwa ngazi ya Stashahada ya Elimu ya Maandalizi, Elimu ya Msingi na Elimu Mjumuisho imeandaliwa na kuidhinishwa kwa ajili ya matumizi.
- ii. Jumla ya vitabu 2,216,540 vya elimu ya Sekondari vimechapishwa na kusambazwa katika skuli za Unguja

na Pemba. Vitabu 1,108,270 vya Kidato cha Kwanza na 1,108,270 vya Kidato cha Pili. Aidha, vitabu 908,184 vya elimu ya Maandalizi na Msingi vikiwemo vitabu 18,000 vya wanafunzi wenyewe mahitaji maalum vimechapishwa kwa ajili ya matumizi katika madarasa ya maandalizi mwaka wa pili, darasa la II na la III.

- iii. Jumla ya walimu 5,879 wa skuli za Serikali na Binafsi wamepatiwa mafunzo ya mtaala mpya. Kati ya hao Walimu 2,878 wa Kidato cha Kwanza, 1,603 wa darasa la sita na 1,398 wa darasa la tatu.

Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu

35. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utoaji wa elimu. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, huduma ya Upimaji na Tathmini ilitengewa ruzuku ya **Tsh. 6,120,400,000**. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 4,604,600,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Tsh. 1,515,800,000** ni kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 6,203,790,961** sawa na asilimia **101** zimepatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 4,781,032,850** sawa na asilimia **104** ni fedha za Matumizi ya Mengineyo na **Tsh. 1,505,800,000** sawa na asilimia **99** ni kwa ajili ya Mshahara. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo:

- i. Jumla ya wanafunzi 61,129 (wanaume 30,982 na wanawake 30,147) wa Darasa la Nne waliandikishwa kufanya Mtihani. Kati ya hao wanafuzi 59,074 (wanaume 29,602 na wanawake 29,476) sawa na asilimia 96.64 walifanya Mtihani huo.
- ii. Darasa la Saba wanafunzi 46,948 (wanaume 22,408 na wanawake 24,540) waliandikishwa kufanya Mtihani.

Kati ya hao wanafunzi 44,486 (wanaume 20,571 na wanawake 23,915) sawa na asilimia 98.03 walifanya Mtihani huo.

- iii. Jumla ya wanafunzi 23,561 (wanaume 12,080 na wanawake 11,481) waliandikishwa kufanya Mtihani wa kumaliza Kidato cha Pili, ambapo wanafunzi 22,424 (wanaume 11,369 na wanawake 11,055) sawa na asilimia 95.17 walifanya Mtihani huo.
- iv. Walimu wanafunzi 1,218 (wanaume 115 na wanawake 1,103) waliandikishwa kufanya mtihani wa Cheti cha Ualimu Maandalizi (CECE), ambapo wanafunzi 1,203 sawa na asilimia 98.77 wamefanya Mtihani huo.
- v. Baraza la Mitihani la Zanzibar (BMZ) limewaandikisha Walimu wanafunzi 840 (wamaume 127 na wanawake 713) wanaotarajiwa kufanya Mitihani ya kumaliza masomo ya Stashahada ya Msingi ya Ualimu katika Vyuo mbali mbali vyta serikali na binafsi Unguja na Pemba, mitihani hiyo imefanyika mwezi huu wa Mei, 2025.

Matokeo ya Muda Mfupi

- i. Jumla ya wanafunzi 55,587 (wanaume 26,896 na wanawake 28,691) wamefaulu mtihani wa Darasa la Nne sawa na asilimia 93.59 ya watahiniwa wote.
- ii. Wanafunzi waliofaulu Mtihani wa kumalizia Darasa la saba ni 44,486 (wanaume 20,571 na wanawake 23,915) sawa na asilimia 96.66 ya watahiniwa wote waliofafanya mtihani huo. Aidha, wanafunzi 5,044 sawa na asilimia 11.34 wamefaulu kuendelea na masomo yao katika madarasa ya Vipawa na Michepuo (Vipawa 228 na Michepuo 4,816).

- iii. Kwa upande wa Kidato cha Pili wanafunzi 18,934 (wanaume 8,905 na wanawake 10,029) sawa na asilimia 84.44 wamefaulu Mtihani huo na kuendelea na masomo ya Kidato cha Tatu.
- iv. Jumla ya Wanafunzi 1,107 (wanaume 103 na wanawake 1,004) sawa na asilimia 90.89 wamefaulu mtihani wa Cheti cha Ualimu Maandalizi (CECE).

Huduma ya Ukaguzi wa Elimu

36. Mheshimiwa Spika, huduma hii ina madhumuni ya kusimamia ubora wa elimu inayotolewa kwa kuhakikisha Sera, Sheria, Miongozo na taratibu zilizowekwa na Serikali zinafuatwa. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, huduma hii ilipangiwa jumla ya ruzuku ya **Tsh. 2,974,700,000**. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 511,900,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Tsh. 2,462,800,000** ni kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 2,293,496,676** sawa na asilimia **77** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 160,700,666** sawa na asilimia **31** ni fedha za Matumizi mengineyo na **Tsh. 2,132,796,013** sawa na asilimia **87** ni kwa ajili ya Mishahara. Utekelezaji wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Wizara imeendelea kutoa ushauri kwa walimu uliozingatia ufundishaji wa mtaala wa umahiri, upimaji endelevu kwa wanafunzi, matumizi ya mbinu sahihi na vifaa, uhuishaji wa paneli za masomo, utoaji mrejesho kwa kazi za wanafunzi na ukamilishaji wa mada katika miutasari.
- ii. Jumla ya washiriki 594 walishiriki katika warsha ya uwasilishaji wa ripoti za matokeo ya upimaji wa kusoma

kuandika na kuhesabu (3K). Shughuli hiyo ilijumuisha Maafisa elimu wa Mikoa na Wilaya, Walimu Wakuu wa skuli za msingi katika Mikoa ya Kaskazini na Kusini Unguja, Kaskazini na Kusini Pemba. Aidha, matokeo yameonesha asilimia 55 ya wanafunzi wameweza kusoma maneno kwa ufasaha, 45 wameweza kuandika maneno na 58 ya wanafunzi wameweza kufanya matendo ya Kihesabu.

- iii. Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu imefanikiwa kufanya marekebisho ya Miongozo ya ukaguzi katika ngazi zote za elimu (Maandalizi, Msingi na Sekondari) kuendana na mahitaji ya Mtaala wa umahiri.
- iv. Wizara imetua mafunzo ya Kanuni za Utumishi wa Umma na Sheria ya Ukaguzi wa Elimu kwa Wafanyakazi 110 Unguja na Pemba. Lengo ni kuwawezesha wafanyakazi kufanya kazi kwa ufanisi.
- v. Jumla ya watendaji wawili wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU) na Chuo cha kuendeleza Taaluma (ICPS). Aidha, Mtendaji mmoja amepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya Uhasibu kuhusiana na Mfumo mpya wa ufungaji wa hesabu (International Public Sector Accounting Standard (IPSAS)).
- vi. Jumla ya watendaji 60 wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu wamehuduria kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mpango kazi wa mwaka 2024/2025 na kujadili mafanikio na changamoto za Ofisi. Vilevile kupendekeza hatua za kuchukua kwa lengo la kupunguza changamoto zilizojitokeza na kuimarisha ufanisi katika kazi.

Matokeo ya Muda Mfupi

- i. Jumla ya skuli 921 (594 za Serikali na 327 za Binafsi) zimekaguliwa kati ya skuli 1,024 zilizokadiriwa kukaguliwa kwa mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 90. Kati ya skuli hizo 87 ni za Maandalizi, 458 za Msingi na 376 za Sekondari. Aidha, skuli 102 zimekaguliwa kwa ajili ya kupatiwa usajili.
- ii. Jumla ya walimu 2,911 wamekaguliwa kati ya walimu 2,900 waliopangwa kukaguliwa kwa mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 100.4

Huduma za Maktaba

- 37. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kuimarisha usomaji kwa kutoa fursa ya kutumia vitabu, nyaraka na nyenzo nyengine za taaluma kwa watoto, wanafunzi wa ngazi zote na jamii. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, huduma hii ilipangiwa kutumia ruzuku ya **Tsh. 6,529,700,000**. Kati ya fedha hizo **Tsh. 878,000,000** ni kwa ajili ya mishahara, **Tsh. 451,700,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Tsh. 5,200,000,000** kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 887,899,967** sawa na asilimia **15** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 854,744,005** sawa na asilimia **97** ni fedha za Matumizi ya Mshahara na **Tsh. 119,591,500** sawa na asilimia **26** ni kwa matumizi Mengineyo. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo:

- i. Wizara imeziimarisha maktaba 19 na kuzipatia vifaa. Kati ya hizo, Maktaba 17 ni za Skuli, maktaba moja ni ya kituo cha Watoto yatima (ZASO) na maktaba ya Hospitali ya Kivunge.

- ii. Jumla ya vitabu 29,463 vimepatikana na kusambazwa katika Maktaba kuu na Maktaba za skuli. Aidha, nakala 2,626 za magazeti zimenunuliwa kwa lengo la kutoa taarifa za matukio mbalimbali.
- iii. Jumla ya wafanyakazi tisa wameshiriki katika mafunzo ya muda mfupi kupitia semina na makongamano, yakiwemo mafunzo ya Ukutubi, usimamizi wa miradi na uongozi. Aidha wafanyakazi wanne wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ngazi ya shahada ya kwanza, wawili wanasomea fani ya ukutubi, mmoja saikolojia na mmoja fani ya utawala.
- iv. Wizara imeendelea na zoezi la kuhamasisha wanafunzi na jamii juu ya matumizi ya maktaba kupitia vyombo vya habari na maonesho. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya watumiaji 48,797 walifika maktaba kupata huduma mbalimbali Unguja na Pemba. Idadi hii inajumuisha watu wazima 22,055 (wanaume 10,871 na wanawake 11,184) na watoto 26,742 (wanaume 13,672 na wanawake 13,070). Aidha, jumla ya wanachama 31 wapya walisajiliwa.
- v. Wizara imeandaa programu 336 zenyе lengo la kuhamasisha matumizi ya maktaba, na kujenga utamaduni wa kusoma vitabu. Programu 36 za vijana, 84 za nje ya maktaba, 98 za watoto (Friday program) na 118 za ziara za Maktaba za wanafunzi kutoka skuli mbalimbali za serikali na binafsi.

Matokeo ya Muda Mfupi

- i. Idadi ya watumiaji wa maktaba imeongezeka kutoka 44,942 mwaka 2024 hadi kufikia 48,797 mwaka 2025.

- ii. Jumla ya magazeti 2,626 na vitabu 29,463 vimepatikana na kusambazwa katika Maktaba kuu na Maktaba za skuli.
- iii. Jumla ya Maktaba 19 zimeimarishwa mwaka 2024/22025 kutoka maktaba maktaba 13 mwaka 2023/2024.
- iv. Jumla ya wanachama wapya waliosajiliwa wameongezeka kutoka 562 mwaka 2024 hadi kufikia 593 mwaka 2025.

Huduma ya Baraza la Elimu

38. Mheshimiwa Spika, huduma hii ina madhumuni ya kuhakikisha Sheria, Sera na Taratibu zilizowekwa na Serikali zinafuatwa katika uendeshaji wa skuli za Serikali na za binafsi. Huduma hii pia inatoa leseni kwa walimu na kuzisajili skuli za Serikali na za binafsi pamoja na vyuo vya ualimu vya kati. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Baraza la Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, huduma hii ilipanganya kutumia jumla ya ruzuku ya **Tsh. 391,300,000**. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 108,900,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Tsh. 282,400,000** ni kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 343,085,731** sawa na asilimia **88** zimepatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 275,935,731** sawa na asilimia **98** ni fedha za Matumizi ya Mshahara na **Tsh. 67,150,000** sawa na asilimia **62** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Jumla ya vyuo viwili vya ualimu vya Binafsi vimewasilisha maombi ya usajili wa fani ya ualimu ambapo chuo kimoja tayari kimepatiwa usajili na kingine bado kinaendelea na taratibu za usajili.

- ii. Jumla ya walimu 6,105 wa ngazi ya Cheti, Stashahada, Shahada ya kwanza na ya Pili walipatiwa leseni za kufundishia za muda wa miaka mitano kutoka skuli za Serikali na Binafsi kwa Unguja na Pemba.
- iii. Jumla ya kesi mbili za ndoa zinazohusisha wanafunzi (mmoja wa Msingi na mmoja wa Sekondari) zimeripotiwa kutoka Wilaya ya Kaskazini B na Wilaya ya Mjini. Aidha, jumla ya kesi 17 za ujauzito zimepokelewa zikiwemo saba Unguja na 10 Pemba. Kesi zote zikiwemo za udhalilishaji, ndoa na ujauzito zimefuatiliwa na kujadiliwa na Maafisa wa Baraza la Elimu na kuwasilishwa Idara ya Elimu Maandalizi na Msingi, Idara ya Elimu Sekondari pamoja na Jeshi la Polisi kwa lengo la kufuatiliwa kwa kina.
- iv. Jumla ya kesi 13 (Tatu Unguja na 10 Pemba) za udhalilishaji zikiwemo ubakaji na ulawiti zimeripotiwa katika ofisi ya Baraza la Elimu.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Jumla ya leseni 6,105 (4,502 Unguja na 1,603 Pemba) za walimu zimetolewa.
- ii. Jumla ya skuli 40 (Unguja 38 na Pemba mbili) za Binafsi zimesajiliwa. Kati ya skuli hizo 22 za maandalizi, 16 za msingi na mbili za sekondari.
- iii. Jumla ya kesi 32 za udhalilishaji zimefuatiliwa na kutolewa maamuzi.

Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu

- 39. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kuifanya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano itumike katika ngazi ya utawala, kujifunza na kufundishia, kuimarisha huduma ya mawasiliano na kutunza usalama

wa taarifa. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Tsh. 17,675,830,698**. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 395,691,698** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Tsh. 580,139,000** ni kwa ajili ya mishahara. Aidha, **Tsh. 16,700,000,000** zilitengwa kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 6,595,651,039** ambazo ni sawa na asilimia **37** zimepatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 523,745,039** sawa na asilimia **90** ni mshahara, **Tsh. 71,906,000** sawa na **18** ni Matumizi ya kawaida na **Tsh. 6,000,000,000** sawa na asilimia **100** ni kwa ajili ya Maendeleo kutoka kwa Wahisani. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Kazi ya kuunganisha Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano (National Fiber Backbone) inaendelea katika hatua za ukamilishaji kwa kuunganisha vituo 100, vikiwemo skuli 70, Vituo vya Ualimu (TC's) 10, Vituo vya Ubunifu wa Kisayansi (hubs) 18, Kituo cha Elimu Mbadala-Unguja na ofisi ya Maktaba-Pemba. Hatua hii imewezesha upatikanaji wa intaneti yenyе kasi kwa matumizi ya kielimu.
- ii. Wizara imekamilisha uandaaji wa Mfumo wa kidijitali wa kujifunzia na kufundishia (LMS) ambao umeundwa mahsus kwa ajili ya kuwawezesha walimu na wanafunzi kushiriki katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa njia ya mtandao. Aidha, mfumo wa ZEAS pamoja na tovuti ya Wizara imeboreshwa ili viweze kufanya kazi kwa ufanisi na usahihi zaidi.
- iii. Wizara imekamilisha ununu zi wa kompyuta 1,500, Projekta 500, kompyuta mpakato (laptop) 500 na seva

- nne kwa ajili ya matumizi ya TEHAMA katika sekta ya elimu hasa katika kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.
- iv. Jumla ya walimu 817 wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji kwa lengo la kubadilisha mbinu za jadi za ufundishaji na kuziimarisha kupitia teknolojia.
 - v. Jumla ya wafanyakazi wanne wa Idara ya TEHAMA wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi juu ya utengenezaji wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA.
 - vi. Wizara kupitia Kituo cha Habari za Elimu Cha Kwarara (KMEC) imeandaa vipindi 72 vya redio vya masomo mbalimbali kwa madarasa tofauti katika ngazi za Elimu ya Maandalizi, Msingi na Sekondari. Aidha, vipindi mbalimbali vya kielimu na kijamii vinaendelea kurushwa kupitia Televisheni yake ya EZTV na Elimu FM Radio. Aidha, Wizara imeandaa vipindi vitatu vya TV vinavyofundisha namna ya kutayarisha vipindi vya Televisheni kuanzia uandishi wa makala, kurekodi pamoja na kuhariri picha.
 - vii. Jumla ya vipindi tisa vya TV vya somo la Dini ya Kiislam kwa wanafunzi wa ngazi ya elimu msingi na vipindi 3 vya TV vya ofisi ya Mufti vyenye maudhui mbalimbali vimeandaliwa. Aidha, programu 15 za TV za lugha ya alama kwa wanafunzi wenyewe mahitaji maalum zimeandaliwa. Lengo la programu hizi ni kuwasaidia walimu na wanafunzi wenyewe mahitaji maulum kwa upande wa usikivu hafifu ili kufahamu mambo mbalimbali katika masomo yao.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Idadi ya walimu waliopatiwa ujuzi wa TEHAMA kwa mwaka imeongezeka kutoka 223 mwaka 2023/2024 hadi kufikia 817 mwaka 2024/2025.
- ii. Idadi ya Skuli zilizounganishwa na Mkonga wa taifa zimeongezeka kutoka skuli 3 mwaka 2023/24 hadi kufikia skuli 70 mwaka 2024/25. Aidha jumla ya vituo 18 vya ubunifu wa kisayansi (Hubs), Vituo 10 vya walimu (TCs), Ofisi ya Maktaba Pemba na Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo vimeunganishwa Mkonga wa Taifa.

Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha

40. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa elimu kwa watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalum. Programu hii inatekelezwa na Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 programu hii ilitengewa jumla ya **Tsh. 195,000,000** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Aprili, 2025, jumla ya **Tsh. 76,500,000** sawa na asilimia **39** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ndogo ni kama ifuatavyo: -

- i). Wizara imefanya ufuatiliaji katika skuli 46 za msingi na sekondari kwa lengo la kuangalia masuala ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha pamoja na kuwatambua wanafunzi wenye mahitaji maalum na kuona changamoto zinazowakabili wanafunzi hao mashulen. Aidha, katika ufuatiliaji huo wanafunzi 48 waligundulika na changamoto na kupatiwa vifaa saidizi. Vifaa vilivyotolewa ni viti vya maringi mawili, mashine za nukta nundu, karatasi za kuandikia maandishi ya nukta nundu, mashine za kurikodia sauti (voice recorder). Aidha, jumla ya skuli 28 za elimu mjumuisho

zimepatiwa vifaa saidizi na vifaa vya kujifunzia na kufundishia ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji.

- ii). Wizara imefanya Makongamano mawili ya kuadhimisha siku 16 za harakati za kupinga vitendo vya Udhailishaji kwa wanawake na watoto. Jumla ya washiriki 209 (82 wanaume na 127 wanawake) wameshiriki kutoka katika skuli 15 za Msingi na Sekondari.
- iii). Wizara ilifanya maadhisho ya miaka 20 tokea kuanzishwa Elimu Mjumuisho Zanzibar. Jumla ya washiriki 300 walihudhuria kutoka Unguja, Pemba na Tanzania Bara.
- iv). Jumla ya maafisa 25 (21 wanawake na 4 wanaume) wa elimu mjumuisho walijengewa uwezo wa kuwatambua kwa usahihi wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
- v). Jumla yawanafunzi 185 (75 wanaume na 110 wanawake) kutoka skuli 12 za sekondari Unguja wameshiriki katika mafunzo ya uchaguzi wa kazi (Career guidance).

Matokeo ya muda mfupi

- i. Jumla ya walimu 1,066 (wanawake 799 na wanaume 267) wamepatiwa mafunzo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha mwaka 2024/2025.
- ii. Jumla ya wanafunzi 10,269 wenye mahitaji maalumu wameandikishwa katika skuli za Serikali na Binafsi.

Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni

- 41. Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mwanafunzi kimwili, kiafya na kiakili katika kujifunza kwa kupitia michezo. Shughuli za programu hii zinatikelezwa na Idara ya Michezo na Utamaduni katika elimu. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Tsh. 2,080,131,698**. Kati ya

fedha hizo, **Tsh. 1,080,131,698** ni kwa matumizi ya kazi za kawaida kati ya fedha hizo, **Tsh. 615,691,698** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Tsh. 464,440,000** ni kwa matumizi ya mishahara na **Tsh. 1,000,000,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 667,477,908** sawa na asilimia 32 zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 322,943,310** sawa na asilimia **70** ni fedha ajili ya Mshahara na **Tsh. 344,534,598** sawa na asilimia **56** za Matumizi ya Mengineyo. Utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Wizara imeadhimisha miaka 60 ya Elimu bila ya Malipo mnamo mwezi wa Septemba 2024.
- ii. Jumla ya walimu 85 (wanaume 52 na wanawake 33) wa michezo na utamaduni kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya michezo na sanaa yakiwemo mafunzo ya mpira wa kikapu, wavu na mpira wa mikono, mafunzo ya michezo ya utamaduni. Pia, Wizara imeendeleza mashirikiano na Chama cha Skauti Tanzania (TSA) katika kusimamia shughuli mbalimbali za kitaifa.
- iii. Wizara imetoa mafunzo ya mpira wa kikapu, wavu na pete kwa walimu 48 (wanaume 21 na wanawake 27) na afisa mmoja wa Idara ya Michezo na Utamaduni katika Elimu.
- iv. Wizara kwa kushirikiana na watu wenye asili ya Tanzania wanaoishi ughaibuni (Diaspora) wametoa mafunzo ya ukocha wa mpira wa miguu kwa walimu 15 wa skuli za Msingi na Sekondari. Aidha, jumla ya walimu 1,510 (966 wanawake na 544 wanaume) wamepatiwa mafunzo ya kuogelea na usalama katika maji kwa walimu kutoka skuli za Msingi na Sekondari kwa mafunzo ya nadharia

(Theory) na walimu 22 (8 wanaume na 14 wanawake) walipatiwa mafunzo ya kuogelea kwa vitendo kwa Unguja na Pemba.

- v. Wizara inaendelea na mchakato wa ujenzi wa viwanja vitatu vya skuli za Fidel-Castro, Paje Mtule na Mambosasa kwa lengo la kuimarisha michezo katika elimu. Kwa sasa hatua ya michoro na BoQ tayari imeshakamilika.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Mashindano ya michezo mbalimbali na sanaa yamefanyika kuanzia ngazi ya kanda hadi Taifa. Aidha, jumla ya wanafunzi 778 (wanaume 370 na wanawake 408) wenyе vipaji vya michezo na utamaduni wameshiriki katika michezo hiyo.
- ii. Jumla ya walimu 500 kutoka skuli za msingi na sekondari wamepatiwa taaluma ya michezo na utamaduni ambapo walimu 222 wanawake na 278 wanaume.
- iii. Jumla ya skuli 30 za Msingi na Sekondari zimepatiwa mipira ya michezo wa mpira wa miguu.

PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI

- 42. Mheshimiwa Spika**, Programu ya Utawala na Uongozi ina lengo la kuhakikisha usimamizi wa matumizi na upatikanaji wa rasilimali bora katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya elimu. Programu hii ina programu ndogo tatu zikiwemo Programu ndogo ya Uongozi kwa Ujumla, Programu ndogo ya shughuli za Mipango, Sera na Utafiti na Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za Elimu Pemba. Programu hii ilipangiwa jumla ya **Tsh. 51,808,137,918**. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 11,878,387,918** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Tsh. 9,579,750,000** ni kwa ajili ya mishahara

na **Tsh. 30,350,000,000** ni kwa ajili ya kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 18,115,068,490** sawa na asilimia **35** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 15,543,734,585** sawa na asilimia **72** ni fedha za Matumizi ya Kawaida zikiwemo **Tsh. 9,080,204,676** sawa na asilimia **95** kwa ajili ya Mshahara na **Tsh. 6,463,529,909** sawa na asilimia **54** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. **Tsh. 2,571,333,904** sawa na asilimia **8** ni kwa ajili ya Maendeleo ambapo **Tsh. 1,899,520,971** sawa na asilimia **9** ni kutoka SMZ na **Tsh. 671,812,933** sawa na asilimia **7** ni kutoka kwa wahisani.

Programu ndogo ya Uongozi kwa Ujumla

43. Mheshimiwa Spika, programu hii ina madhumuni ya kuhakikisha ufanisi wa Uongozi na Utawala wa rasilimali za Wizara. Shughuli za programu hii ndogo zinatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, programu hii ilipangiwa jumla ya **Tsh.16,146,948,416**. Kati ya fedha hizo, **Tsh.7,674,402,416** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Tsh.7,472,546,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Tsh. 1,000,000,000** kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 12,571,503,728** sawa na asilimia **78** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 7,150,986,417** sawa na asilimia **96** ni fedha kwa ajili ya Mshahara na **Tsh. 5,420,517,311** sawa na asilimia **71** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Utekelezaji wa kazi za programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i. Jumla ya wafanyakazi 253 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu, kati yao 190 Unguja na 63 Pemba. Aidha, jumla ya wafanyakazi 25 walipata fursa ya mafunzo ya muda mfupi ya kujengewa uwezo katika kazi zao.

- ii. Jumla ya Tsh. 1,881,200,000 za ubani wa ufiwa zimelipwa kwa wafanyakazi 445 (Unguja 309 na 136 Pemba) na jumla ya wafanyakazi 143 wamelipwa posho la likizo kama moja ya stahiki zao katika utendaji. Aidha, Jumla ya deni la TSh 474,570,000 limelipwa kwa walimu 51 kama ubani na walimu 1,659 kama nauli kwa walimu waliokuwa ugatuza.
- iii. Jumla ya wafanyakazi 1,676 (427 wanaume na 1,249 wanawake) wameajiriwa, Aidha Wafanyakazi 272 wamestaafu kazi kwa mujibu wa sheria, Pia Wafanyakazi wawili wamestaafu kwa hiari. Wafanyakazi wanne wamechukua likizo bila ya malipo, wafanyakazi wanne wamestaafu kwa ugonjwa, na wafanyakazi saba wamefariki dunia, Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi Amiin.
- iv. Wizara inaendelea kuimarisha huduma ya Ulinzi katika Ofisi za Wizara na Skuli. Jumla ya TSh 2,504,674,400 zimelipwa kwa wakala wa Ulinzi (JKU) na UMAWA.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Ufanisi katika utoaji wa huduma, Uongozi na Utawala umeimarika katika ngazi zote na hivyo kupelekeea kuimarika katika utekelezaji wa malengo ya elimu.
- ii. Jumla ya walimu wapya 1,676 wakiwemo walimu 427 wanaume na walimu 1,249 wanawake wameajiriwa kwa Unguja na Pemba.

Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

- 44. Mheshimiwa Spika**, Madhumuni makubwa ya Programu hii ni kufanikisha na kuratibu utekelezaji wa Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka wa fedha

2024/2025, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Tsh. 33,916,292,804**. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 3,658,293,804** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Tsh. 907,999,000** ni kwa ya ajili ya mishahara ya wafanyakazi na **Tsh. 29,350,000,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2025, Jumla ya **Tsh. 4,318,674,104** sawa na asilimia **13** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 1,747,340,199** sawa na asilimia **38** ni fedha za Matumizi ya Kawaida zinazojumuisha **Tsh. 844,015,100** sawa na asilimia **93** ni kwa ajili ya Mshahara na **Tsh. 903,325,099** sawa na asilimia **25** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo. **Tsh. 2,571,333,904** sawa na asilimia **9** ni kwa ajili ya Maendeleo ambapo **Tsh. 1,899,520,971** sawa na asilimia **10** ni kutoka SMZ na **Tsh. 671,812,933** sawa na asilimia **7** kutoka kwa wahisani. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama hivi ifuatavyo: -

- i. Wizara imezindua mfumo wa kukusanya takwimu za Elimu. Aidha, Jumla ya walimu 909 (Pemba 394 na Unguja 515) wa skuli za Serikali za Maandalizi, Msingi na Sekondari wamepatiwa mafunzo ya Mfumo wa Kukusanya Takwimu za Elimu (SIS) kwa Skuli za Unguja na Pemba.
- ii. Wizara imeandaa Sera mpya na kuwasilishwa kwa wadau mbalimbali wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Makatibu Wakuu kwa ajili ya kutoa maoni.
- iii. Wizara imenunua na kusambaza samani zikiwemo seti 22,001 za viti na meza za wanafunzi na seti 670 za viti na meza za walimu.
- iv. Wizara imekamilisha ujenzi wa Skuli 10 Unguja na Pemba. Skuli hizo ni Bumbwini Makoba, Bumbwini Misufini, Tumbatu, Chanjaani-Mwambe, Kojani, Ole,

Chumbuni, Kidichi, Mwera na Michakaini. Aidha, Wizara imeweka mawe ya msingi ya ujenzi wa skuli katika maeneo mbalimbali yakiwemo Gamba, Kifundi, Maungani na Chukwani.

- v. Jumla ya washiriki 1,241 wakiwemo Walimu wakuu, washika fedha wa skuli na wenyeviti wa kamati za Skuli katika skuli za Maandalizi na Msingi wamepatiwa mafunzo ya Mpango wa Maendeleo ya Skuli kwa Wilaya zote Unguja na Pemba. Aidha, washiriki 2,553 wakiwemo Walimu wakuu, Walimu wa taaluma na wajumbe wa kamati za Skuli, Maafisa Elimu Wilaya na Wakaguzi wa elimu wamepatiwa Mafunzo ya Mpango wa Mageuzi ya sekta ya Elimu (ZESTP) kwa Wilaya zote za Zanzibar.
- vi. Kitabu cha Takwimu za Elimu (Annual Statistical Abstract 2020 -2024) kimekamilika na tayari data zimewasilishwa kwa wadau mbalimbali. Aidha, zoezi la kukusanya taarifa kwa ajili ya Sensa ya Skuli (Annual School Census) kwa mwaka 2025/2026 limekamilika.
- vii. Jumla ya maafisa 10 walijengewa uwezo katika maeneo mbalimbali yakiwemo Ufutiliaji na Tathmini (3), Fedha na Mipango (3), mafunzo ya lugha ya kupokea wageni (1) na kuandaa bajeti (3).
- viii. Wizara inaendelea kuimarisha ushirikiano na Nchi Wahisani kwa kuhudhuria vikao mbali mbali kwa ajili ya kutimiza dhamira hiyo. Vikao vilivyohudhuriwa vililusisha Nchi zifuatazo: Iran, China, UAE, Iraq, Cuba Uturuki, Italy, Kuwait pamoja na kikao cha Baraza kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA).
- ix. Wizara imeendelea kufutilia na kusimamia utekelezaji wa miradi ya elimu iliyokamilika na inayoendelea.

Miongoni mwa miradi hiyo ni Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu katika elimu, Mradi wa Uimarishaji wa Ubora wa Elimu kuititia Upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, Mafunzo ya Walimu na Matumizi ya TEHAMA na Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu.

Matokeo ya muda mfupi

- i) Ripoti ya utekelezaji na tathmini ya maendeleo ya elimu imeandaliwa.
- ii) Mapendekezo ya miradi mipyä miwili imeandaliwa na kuwasilishwa kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya kupatiwa ufadhilli.

Programu ndogo ya Uratibu shughuli za elimu Pemba

- 45. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina madhumuni ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za elimu kwa upande wa Pemba. Msimamizi Mkuu wa shughuli za programu hii ni Afisa Mdhaminî wa Elimu Pemba. Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya **Tsh. 1,744,896,698** Kati ya fedha hizo, **Tsh. 1,199,205,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Tsh. 545,691,698** ikiwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Tsh. 1,224,890,658** sawa na asilimia **70** zimepatikana. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 1,085,203,159** sawa na asilimia **90** ni fedha za Mshahara na **Tsh. 139,687,499** sawa na asilimia **26** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Fedha za programu hii zilitumika katika kusimamia na kufuatilia shughuli zote na programu za elimu Pemba.

MAPATO

- 46. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kukusanya

mapato kupitia usajili wa Skuli za binafsi, malipo ya leseni za walimu, ada za usajili wa skuli, ada za kiingilio kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha sita na usajili wa wanafunzi wa skuli binafsi wanaofanya mitihani ya Taifa na usajili wa vituo vya kufanyia mitihani. Hadi kufikia Aprili 2025, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekusanya jumla ya **Tsh. 339,166,764** kati ya **Tsh. 1,140,703,000** zilizopangwa kukusanya. Hii ni sawa ya asilimia **30** ya makadirio. Kati ya mapato yaliyokusanya **Tsh. 128,836,518** zinatokana na malipo ya leseni za walimu, **Tsh. 63,704,247** za malipo ya usajili wa skuli za binafsi, **TSh. 9,250,000** kwa ajili ya malipo ya tenda za wazabuni, **Tsh. 127,195,000** usajili wa wanafunzi wa skuli binafsi wanaofanya mitihani ya Taifa pamoja na usajili wa vituo vya kufanyia mitihani na **Tsh. 10,181,000** za makusanyo ya ada za kiingilio kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha sita.

MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2025/2026 KATIKA MFUMO WA PROGRAMU.

- 47. Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 naomba sasa niwasilishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuzingatia vipaumbele vya Wizara.

Vipaumbele vya Wizara

- 48. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaendelea kutekeleza Mpango wa mageuzi wa sekta ya elimu uliozingatia Mipango ya kitaifa na Kimataifa kwa kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: -

- i. Kuhamasisha jamii katika uandikishaji wa watoto skuli katika umri sahihi, kutoa mashirikiano katika usimamizi wa nidhamu za wanafunzi pamoja na ufuutiliaji wa Maendeleo yao ya skuli.
- ii. Kuimarisha miundombinu ya elimu kwa kuongeza idadi ya madarasa kupitia ujenzi wa skuli 20 za Maandalizi za chini, Skuli 21 za Msingi zinazojumuisha Skuli 16 za ghorofa na skuli 17 za Sekondari, kati ya hizo 12 za ghorofa. Aidha, Wizara inakusudia kujenga skuli tatu za Elimu Mjumuisho katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mjini Magharibi na Mkoa wa Kaskazini Pemba.
- iii. Kufanya ukarabati wa madarasa 900 na kukamilisha madarasa 300 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.
- iv. Kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kujenga vyoo 700 katika skuli za Maandalizi, Msingi na Sekondari, Dakhalia 09, nyumba 10 za walimu, kuziimarisha dakhalia kwa kuziwekea miundombinu ya gesi, kuweka mifumo ya umeme wa jua katika skuli 35 za ghorofa pamoja na kununua samani za skuli zenye ubora.
- v. Kuimarisha Miundombinu ya Ofisi kwa kutanua jengo la Makao Makuu ya Wizara, jengo la Ofisi ya Baraza la Mitihani na Kituo cha Kuchapisha Mitihani, Ofisi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, ujenzi wa chuo cha ubaharia (SUZA), utanuzi wa chuo cha Karume, kujenga Maktaba kuu mpya ya kisasa na Ujenzi wa Chuo cha IIT Madras.
- vi. Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kujifunzia na kufundishia kwa kuzipatia Skuli vifaa vya TEHAMA vikiwemo Smart Screen 25, Kompyuta za Mezani 2,000, Mbao za Mahudhurio za Kidijitali (School Digital-Attendance Board), Laptop 3,000, kuweka vifaa vya

TEHAMA kwa ajili ya Maktaba Mtandao katika skuli 33 za Unguja na Pemba.

- vii. Kuendelea kutekeleza mtaala mpya wa umahiri kwa elimu ya Maandalizi, Msingi na Sekondari kwa kuwapatia walimu mafunzo ya namna bora ya kutekeleza mtaala wa umahiri, kuendelea kuandaa na kuchapisha vitabu vya kiada na viongozi vya Mwalimu ili kusaidia kutekeleza mtaala huu.
- viii. Kuimarisha Mafunzo ya Ufundi na Amali kwa kujenga vyuo vitano vya Mafunzo ya Amali na karakana kwa ajili ya mafunzo ya Amali na Ufundi katika skuli 25 za Sekondari pamoja na kuzipatia vifaa.
- ix. Kuimarisha Michezo na Utamaduni kwa kujenga Sport Academy na viwanja viwili vya michezo vya kisasa katika skuli zenye michepuo ya michezo na kuzipatia skuli vifaa.
- x. Kuimarisha Elimu ya Juu kwa kuongeza fursa ya upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kuanzia ngazi ya Diploma.

- 49. Mheshimiwa Spika**, Sasa naomba kuwasilisha mpango wa Utekelezaji wa maendeleo ya elimu kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa mfumo wa programu kama ifuatavyo: -
- 50. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaendelea kutekeleza malengo yake yaliyozingatia malengo ya Taifa ya Dira ya Maendeleo ya Taifa (2050), Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG), Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Elimu Zanzibar 2023 – 2030 (ZESTP), Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na mikakati mengine ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kuimarisha upatikanaji

wa huduma bora ya elimu nchini. Wizara pia, itaendelea kushirikiana na sekta nyengine zinazotoa huduma za jamii na kuimarisha uchumi ikiwemo Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Maji na Nishati na Madini, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalumu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha Wizara itaendeleza mashirikiano na washirika wa maendeleo wa ndani na nje na mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi kwa ujumla katika utekelezaji wa mpango wake kupitia programu sita na miradi mbalimbali ya maendeleo ya elimu.

- 51. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara itatekeleza miradi mitatu ya maendeleo ambayo ni:-
- I. Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya elimu
 - II. Mradi wa Uimarishaji wa Ubora wa Elimu
 - III. Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu.

MAELEZO YA PROGRAMU ZA ELIMU

- 52. Mheshimiwa Spika,** yafuatayo ni maelezo ya programu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yanayohusisha Madhumuni, Matokeo ya muda mfupi, Viashiria na Shabaha za utekelezaji kwa kila programu.

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

- 53. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mtoto kimwili na kiakili kwa ajili ya kupata elimu ya maandalizi na msingi na kumuwezesha kujuua kusoma, kuandika na kuhesabu na kumtayarisha kwa elimu

ya Sekondari. Jumla ya **Tsh. 250,051,036,000** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 122,084,586,000** ni kwa kazi za kawaida na **Tsh. 127,966,450,000** kwa kazi za maendeleo.

Matokeo ya muda mfupi

- Wanafunzi waweze kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Viashiria vya matokeo

- Asilimia ya uandikishaji.
- Uwiano wa walimu kwa wanafunzi.
- Uwiano wa wanafunzi kwa darasa.
- Asilimia ya Skuli zinazoendeshwa kwa mtindo wa shifti moja

Shabaha ya Utekelezaji

- Kuungeza kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa maandalizi kutoka asilimia 82.5 kwa mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 86.1 mwaka 2026.
- Kuandikisha wanafunzi wenyewe umri sahihi katika ngazi ya elimu ya msingi kufikia asilimia 101.5 mwaka 2026.
- Kupungua kwa uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu kwa ngazi ya maandalizi kutoka 27 mwaka 2025 hadi 25 mwaka 2026.
- Kupungua kwa uwiano wa idadi ya walimu kwa Wanafunzi ngazi ya msingi kutoka 39 Mwaka 2025 hadi 38 mwaka 2026.
- Kupungua kwa Uwiano wa wanafunzi kwa darasa ngazi ya msingi kutoka 57 Mwaka 2025 hadi kufikia 55 Mwaka 2026.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI

- 54. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Elimu ya Sekondari madhumuni yake makubwa ni kumtayarisha mwanafunzi aweze kuendelea na masomo katika ngazi za juu zaidi.

Jumla ya **Tsh. 306,480,272,000** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 124,082,158,000** ni kwa kazi za kawaida na **Tsh. 182,398,114,000** kwa kazi za maendeleo.

Matokeo ya muda mfupi

- Kutoa Elimu ya Sekondari kuongeza kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika ngazi zote.

Viashiria vya matokeo

- Asilimia ya uandikishaji
- Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika ngazi ya Kidato cha Nne na Sita.
- Uwiano wa Wanafunzi kwa mwalimu.
- Uwiano wa wanafunzi kwa darasa.

Shabaha za utekelezaji

- Kuongezeka kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa Sekondari ya awali (Kidato cha 1 – 4) kutoka asilimia 68.2 mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 70.5 mwaka 2026.
- Kuongeza kiwango cha ufaulu cha Wanafunzi wa kidato cha nne kutoka asilimia 82 mwaka 2024 hadi kufikia asilimia 87 ifikapo mwaka 2025.
- Kiwango cha ufaulu cha Wanafunzi wa kidato cha Sita kutoka asilimia 99.9 mwaka 2024 hadi kufikia asilimia 100 mwaka 2025.
- Kubaki na Uwiano wa wanafunzi 45 kwa darasa kwa mwaka 2026.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

55. **Mheshimiwa Spika**, programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujajiri au kuajiriwa. Jumla ya **Tsh. 157,267,238,000** zimepangwa

kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 38,123,569,000** ni kwa kazi za kawaida na **Tsh. 119,143,669,000** kwa kazi za maendeleo. Programu hii ina programu ndogo moja na maeneo matano ya huduma ambayo ni: -

Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu

56. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kuwawezesha walimu kuwa wabunifu, wataalamu na wenye uwezo wa kuongoza ili kukuza ubora wa elimu.

Matokeo ya muda mfupi

